SEHEMU A
Muda: Dakika 15 kwa kila mwanafunzi

Sehemu A inatathmini Stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi matatu:

i. Mazungumzo ya ana kwa ana

ii. Ufahamu wa Kusikiliza

iii. Kusoma kwa sauti

Maagizo ya jumla

1 Mwalimu awafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa tathmini ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.

2 Mwalimu awafahamishe wanafunzi wote kwamba karatasi hii ina mazoezi matatu:

i. Mazungumzo ya ana kwa ana

ii. Ufahamu wa Kusikiliza

iii. Kusoma kwa Sauti

3 Mwanafunzi aandaliwe kiti au dawati kutazamana na mwalimu.

4 Mwalimu atangulize kila zoezi na amfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.

5 Mwalimu amfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.

6 Mwalimu atathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia pamoja na kuweka rekodi.